**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MKOA WA MARA**
**Anuani ya Simu: "REGCOM".**
**Simu Nambari 028/2622004/2622005**
**Fax 028-2622764/2622324**
**E-mail: ras.mara@tamisemi.go.tz**
**Tovuti : www.mara.go.tz**

**OFISI YA MKUU WA MKOA,**
**S. L. P. 299,**
**MUSOMA,**
**TANZANIA.**

# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Ndugu Wananchi, napenda kutoa taarifa ya uzinduzi wa zoezi la unyunyiziaji kiuatilifu cha ukoko majumbani (Indoor Residual Spray Insecticide) kwa lengo la kuua Mbu waenezao malaria kwa mwaka 2018 katika Mkoa wetu wa Mara.

Ndugu Wananchi Mkoa wetu wa Mara ni kati ya Mikoa ya Kanda ya Ziwa yenye maambukizi ya juu ya ugonjwa wa Malaria. Kwa miaka ya nyuma tumeshuhudia milipuko ya ugonjwa wa Malaria ambao uliambatana na vifo vya kina mama wajawazito na kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano katika utafiti ulliofanyika mwaka 2015/2016 ulionesha kuwa kiwango cha maambukizi ya Malaria kwa watoto chini ya miaka mitano katika mkoa wa Mara ulikua asilimia 26.

Baada ya unyunyiziaji 2016/2017 kiwango cha maambikizi kimeshuka hadi asilimia 19. Kiwango hichi bado kiko juu ya wastani wa maambukizi ya malaria kiataifa ambayo ni asilimia 14.9. Hata hivyo katika Halmashauri ya Musoma DC kulikua na wagonjwa 82,504 kabla ya zoezi na 8085 baada ya zoezi kwa mwaka vivyo hivyo kwa Wilaya ya Butiama kabla ya zoezi

wagonjwa walikua 59,768 na baada ya zoezi walikua 3563. Haya nimafanikio makubwa.

Ndugu Wananchi, kufuatia hali hiyo, Serikali imekua ikichukua hatua mbalimbali zikiwemo tiba sahihi kwa wagonjwa kwa kutoa Dawa ya Mseto, pia imegawa vyandarua vyenye kiuatilifu vipatavyo 297,240 katika Mkoa wa Mara kwa wanafunzi wa sule za Msingi, ugawaji wa vyandarua kwa mama wajawazito wanaofika kliniki kwa hudhurio la kwanza na watoto chini ya mwaka mmoja unaendelea. Sambamba na ugawaji wa vyandarua, Mkoa pia imenyunyizia viuadudu kwenye mazalia ya mbu katika Halmashauri 7 za Mkoa wa Mara kati ya Halimashauri 9 kutumia viuadudu sehemu ya lita 7940 ambazo zilitolewa na Mh. Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

Vilevile unyunyiziaji wa kiuatilifu ukoko majumbani (Indoor Residual Spray Insecticide) utachangia pia katika juhudi zote za kupambana na Mbu waenezao Malaria. Matokeo ya kazi hii kubwa ni kwamba kutakua na punguzo kubwa la maambukizi ya wagonjwa wa Malaria.

Ndugu Wananchi unyunyiziaji wa viuatilifu ya ukoko vya kuua mbu majumbani (Indoor Residual Spray insecticides) unatekelezwa na Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na shirika la Abt Associates chini ya ufadhili wa Serikali ya Marekani, kupitia Shirika la Misaada na Maendeo la watu wa Marekani (USAID), huu ni mpango wenye gharama kubwa na wenye matokeo ya haraka katika kudhibiti ugonjwa wa Malaria. Kwa wastani upuliziaji kiuatilifu cha ukoko cha kuua mbu majumbani hugharimu takribani kiasi cha shilingi Tshs. 5.4 Bilioni.

Ndugu Wananchi, kwa mwaka huu 2018, unyunyiziaji utafanyika katika Halmashauri za Wilaya za Musoma na Butiama kuanzia tarehe 14 Februari 2018 hadi tarehe 13 Machi 2018. Kwa mwaka huu tunalenga kunyunyizia nyumba zipatazo 105,788 katika Halmashauri hizo mbili zilizotajwa. Kazi hii ya unyunyiziaji itatekelezwa na wananchi wenyewe katika maeneo yao na wanyunyiziaji wapatao 1341 kwa kusimamiwa na viongozi wa Serikali kuanzia ngazi ya Mkoa hadi Vitongoji hivyo pamoja na kupambana na ugonjwa wa Malaria,  zoezi hili pia ni fursa ya ajira kwa wananchi wetu.

Ndugu Wananchi, wito wangu ni kwa wananchi wa Wilaya zilizotajwa hapo juu kutoa ushirikiano wa hali ya juu, hasa kwa viongozi wa kaya kuandaa nyumba zao na kutoa ushirikiano kwa wanyunyiziaji kwa maeneo yote yatakayonyunyiziwa kiuatilifu ukoko ili zoezi hili liweze kufanikiwa kwa kiwango kikubwa na kufikia lengo la nyumba 105,788 na kutokomeza kabisa maambukizi ya ugonjwa wa Malaria katika Halmashauri husika.

Ndugu Wananchi, Kwa bahati mbaya juhudi hii kubwa ya serikali pia hukumbana na hujuma zilizoegemea kwenye Ujinga na Imani potofu. Zoezi hili wilaya ya Rorya mwaka 2013 lilikumbana na jitihada za makusudi za baadhi ya watu kuhujumu kazi ya unyunyiziaji baada ya wananchi na wataalamu kwa pamoja kunyunyizia kiuatilifu ukoko majumbani (Indoor Residual spray Insecticide). Waharibifu hao walikua wakieneza taarifa za uwongo zenye upotoshaji wa kwamba unyunyiziaji huu ulikua unasababisha athari za mwili ikiwemo kupunguza nguvu za kiume na kuondoa hamu ya tendo la ndoa kwa wanawake. Upotoshaji huo hauna misingi ya kisayansi badala

yake Wilaya ya Rorya ambayo ilikua imeanza kushusha matukio ya maambukizi sasa imeanza kupandisha tena.

Ndugu Wananchi, Nawaagiza viongozi wote kuanzia ngazi ya kitongoji, Kijiji, Kata, Tarafa na Wilaya kushiriki kikamilifu katika zoezi la unyunyiziaji wa kiuatilifu cha ukoko cha kuua Mbu waenezao Malaria majumbani kwa kuhamasisha wananchi pamoja na kushughulikia kwa haraka vitendo vyoyote vya hujuma dhidi ya zoezi hili muhimu.

Aidha, naviagiza vyombo na kamati zote za ulinzi na usalama kushirikiki kikamilifu katika zoezi hili na kuwa macho na vitendo vyovyote vya hujuma kama wizi wa viuatilifu ili vyombo hivyo viweze kutoa msaada wa haraka na kudhibiti hujuma hizo.

Ndugu Wananchi, Mwisho niwaombe tena kutoa ushirikiano mkubwa katika zoezi hili muhimu ili kuutokomeza kabisa ugonjwa wa malaria Mkoa wetu wa Mara. Aidha nisisitize kuwa zoezi hili linaanza kesho Februari 14, 2018 mimi mwenyewe Mkuu wa Mkoa pamoja na Ofisi yangu tutafanya ufuatiliaji wa karibu sana kuhakikisha zoezi linafanikiwa na tunafikia lengo kwa asiliamia 100%.

**Mara bila Malaria inawezekana;**

Mhe. Adam Kighoma Ali Malima
**MKUU WA MKOA**
**MARA**
13/02/2018